



EAST AFRICAN
**CRUDE OIL
PIPELINE**

OMBI LA KUONYESHA NIA: KUBUNI NA KUTEKELEZA PROGRAMU YA KUREJESHA MBINU ZA KUPATA MAHITAJI YA MAISHA KUPITIA UVUVI NA BAHARI KWA AJILI YA JAMII ZA WAVUVI ZA MKOA WA TANGA.

REJEA: 00000027

EACOP Ltd (Kampuni) Tanzania, kampuni ya mafuta na Gesi, inaalka taasisi zenye uzoefu na sifa kuonyesha nia ya kutoa huduma ya kuandaa, kusimamia na kutekeleza "Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha Kupitia Kuvua na Uvuvi wa Baharini" ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na kusafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania.

MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA:

Kituo cha baharini cha Mradi wa EACOP kilichopo katika Rasi ya Chongoleani, kinajumuisha hifadhi ya baharini ya kituo cha mwisho (Marine Storage Facility), gati yenye kilomita 2 na kituo cha kushushia mizigo. Shughuli za uvuvi za jamii za eneo hilo zitaathiriwa na ujenzi na uendeshaji wa gati ambayo inawezekana ikajumuisha eneo hilo kufanywa kuwa ukanda uliotengwa, ambao vyombo vya uvuvi havipaswi kuwepo

Mpango Kazi wa Uhamishaji watu na Makazi (Resettlement Action Plans) wa nyongeza na Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha vimebuniwa na ukusanyaji wa taarifa za ziada unaendelea ili kuifanua programu zaidi. Mtaa mmoja utaathiriwa zaidi, mtaa wa pili utaathiriwa kiasi na mitaa mingine miwili itaathiriwa.

Kampuni/watoa huduma ya ushauri/taasisi ya wataalamu, inahitajika kufanya ubunifu wa kina na kutekeleza programu ya uvuvi/Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha Kupitia bahari ikijumuisha ketengo kinacholenga kaya zilizoguswa na mradi na kitengo kinacholenga jamii nzima

VIGezo MUHIMU VYA KUZINGATIA:

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

1. Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana na utekelezaji wa programu za uendelezaji uvuvi, programu za uvuvi za kijamii na mbinu za kupata mahitaji ya maisha kupitia bahari (mfano kukusanya mazao ya bahari, kuvua, nakadhalika) ndani ya Tanzania
2. Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
3. Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kutekeleza programu za uendelezaji uvuvi, programu za uvuvi za kijamii na mbinu za kupata mahitaji ya maisha kupitia bahari (mfano kukusanya mazao ya bahari, kuvua, nakadhalika) na uzoefu wa kufanya kazi na jamii zinazotegemea mbinu za kupata mahitaji ya maisha kupitia bahari.
4. Mifano ya kazi zinazoonyesha uzoefu wa kufanya kazi zinazofanania na hizo zilizofanywa kipindi cha karibuni, ndani miaka mitano iliyopita toka siku ya tangazo hili
5. Wafanyakazi wataopendekezwa kufanya kazi kwenye mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
6. Uthibitisho wa kusajiliwa ndani ya kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi au udhibitisho kuwa wa maombi ya kusajiliwa katika kanzi data yameidhinishwa wakati wa kuwasilisha ombi la kuonyesha nia.
7. Mwombaji azingatie Kanuni ya Sekta ya Petroli ya Ushirikishwaji wa Wazawa/Ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa procurement.tz@eacop.com (ukubwa wa barua pepe **20 Mb**) saa au kabla ya **saa tisa mchana saa za Afrika Mashariki (EAT) tarehe 23 Nov. 2022**. Kichwa cha barua pepe kiwe ni **00000027**.

Muhimu: Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwiliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.